
: © ActionAid

# Janga Lisilo na Usawa

## Ufahamu na Uthibitisho kutoka kwa Jamii na Mashirika ya Asasi za Kiraia

**Muhtasari**

## Kuhusu ripoti hii

The Civil Society Collaborative on Inclusive COVID-19 (Ushirikiano wa Asasi za Kiraia katika Data Inayojumuisha ya COVID-19) inatafuta kusitawisha uwezekano wa data iliyotokezwa na jamii na Civil Society Organisations (CSOs) (Mashirika ya Asasi za Kiraia). Ushirikiano huu unalenga kuunda uelewaji wa jumla wa jinsi watu ambao wametengwa wameathiriwa na janga la COVID-19, itikio na ustahimilivu wao.

Ushirikiano huu unatokana na wakati na juhudi za jamii na mashirika mengi katika kipindi chenye changamoto kubwa.  Tunatoa shukrani kwa watu binafsi, vikundi na jamii ambazo zimechangia kwa ukarimu maoni na mambo waliyoshuhudia kwa utafiti uliochangia ripoti hii.

Zaidi ya CSOs 20 zinajihusisha na Ushirikiano huu, zikiwakilisha na kufanya kazi na vikundi mbalimbali, kutia ndani: makabila madogo; Daliti; watu wa asili; wakimbizi wa ndani; shoga wa kike,  shoga wa kiume, wanaovutiwa kingono na watu wa jinsia zote mbili, waliobadili jinsia zao, ushoga na walio kati ya jinsia zote;  wahamiaji;  watu wenye umri mkubwa zaidi;  walemavu; wakimbizi; dini ndogondogo; watoto wa mitaani; watu wasio na hati; wanawake na wasichana; na vijana.

The Global Partnership for Sustainable Development Data (GPSDD) (Ushirikiano wa Ulimwengu kwa ajili ya Data ya Maendeleo Endelevu) na International Civil Society Centre (ICSC) (Kituo cha Kimataifa cha Asasi za Kiraia) zilishiriki jukumu la ukatibu kwa niaba ya Ushirikiano huu, zikileta pamoja mtandao wa washirika wawili wa GPSDD's Inclusive Data Charter (Mkataba wa Data Inayojumuisha wa GPSDD) na Ushirikiano wa International Civil Society Centre (ICSC) wa Leave No One Behind (Usiache Yeyote Nyuma).

*Publicado e Iliyochapishwa mnamo Julai 2021*

# Muhtasari wa Jumla

**Watu ambao wametengwa wametoa mchango muhimu kwa itikio la janga la COVID-19: kuandaa msaada wenye manufaa kwa familia, marafiki na marika (kutia ndani vifurushi vya chakula); kuandaa msaada wa kifedha kwa pande zote; na kutafsiri au kushiriki habari rasmi. Watu ambao wametengwa wamedhihirisha ustahimilivu usio wa kawaida, kubadilikana na athari za janga, kutia ndani kutafuta vyanzo badala vya mapato.**

Kinyume na jitihada za jamii, maitikio rasmi ya serikali kuelekea COVID-19 kwa kawaida yamepuuza au kutohusisha watu ambao wametengwa. Janga hili limefunua mapengo makubwa na upendeleo katika data rasmi zinazochapishwa na kutumiwa na mashirika ya serikali na mabaraza ya kitaifa. Mapengo haya ya data yanawafanya watu na vikundi vingi 'kutoonekana', na hivyo kutowahusisha katika maitikio ya kitaifa. Janga hili limejenga juu ya miundo ya ukosefu wa usawa wa jamii zetu, likiathiri watu ambao wametengwa kwa kiwango kisichowiana.

Maitikio ya janga la COVID-19 yenye matokeo na maponyo yanahitaji uelewaji wa kina wa athari za COVID-19 kwa watu ambao wametengwa na mikakati inayotumiwa na jamii kubadilikana na kudhibiti athari hizi. Data zinazokusanywa na jamii na Civil Society Organisations (CSOs) (Mashirika ya Asasi za Kiraia) zinaweza kuongeza uwezo wa kuonekana kwa watu na vikundi vilivyopuuzwa na data rasmi, kuboresha uelewaji wa hali zao na mikakati ya kukabiliana.

Ili kuelewa matokeo yasiyo na usawa ya janga la COVID-19 na kutengeneza njia ya kufikia maponyo yanayojumuisha, kikundi cha CSO kiliunda The Civil Society Collaborative on Inclusive COVID-19 Data (Ushirikiano wa Asasi za Kiraia katika Data Inayojumuisha ya COVID-19). Kwa kufanya kazi pamoja na jamii, Ushirikiano huu unatetea mtazamo wa jumla zaidi unaothamini kutumia data ya jamii na CSO kusaidia kukimu mahitaji mbalimbali ya watu na vikundi ambavyo vimetengwa. Ripoti hii inatumia ufahamu kutoka kwa data za jamii na CSO zilizokusanywa na washirika wa Ushirikiano, kwa kawaida kwa ushirikiano wa karibu na jamii, ili kuandaa picha iliyo wazi zaidi ya athari za janga la COVID-19 kwa watu ambao wametengwa na maitikio yao. Ripoti hii inaangazia masuala matano ya kawaida na athari kwa watu ambao wametengwa: ufikiaji wa afya; mapato na riziki; ukosefu wa usalama wa chakula; elimu; na ukatili, unyanyasaji na ubaguzi.

Ripoti hii haikusudiwi kuandaa picha ya kina ya hali halisi zinazopitiwa wakati wa janga na watu ambao wametengwa au kukosoa kupita kiasi maitikio ya serikali kuelekea COVID-19. Badala yake, zingatio ni katika kutumia ufahamu kutoka kwa data ya jamii na CSO kuchochea maitikio na maponyo ya janga la COVID-19 yanayojumuisha zaidi na kudhihirisha thamani ya data hii.

Ufahamu katika ripoti hii unaangazia kwamba data rasmi huandaa picha isiyotosheleza ya jamii inayoshuhudia kutengwa katika janga hili. Ufahamu pia unaashiria changamoto kubwa mno ambazo watu ambao wametengwa wamelazimika kuitikia, kwa kawaida bila utegemezo wa kutosha kutoka kwa serikali.

# Sauti za Jamii

**Kwa maneno yao wenyewe, watetezi wanne wa jamii wanashiriki mawazo yao kuelekea athari za janga, maitikio ya jamii zao, na tamaa zao kwa ajili ya ripoti hii.**

---

**Daniel Calarco,**
wakili mwenye umri wa miaka 24, kiasili kutoka Vila do Vintém Favela iliyo Rio de Janeiro, Brazil.



"Ili kujenga upya kwa njia endelevu, tunahitaji kwanza kuelewa jinsi janga hili limeathiri jamii zetu na vipaumbele vyao kwa wakati ujao. Tunaweza tu kujua hili ikiwa tuna data inayofaa. Data ambayo inakutanisha, inayothamini na kuhalalisha ujuzi wa kienyeji. Data inayokusanywa na kufuatiliwa na jamii kwa usalama, pamoja na data inayolinda jamii kutokana na matumizi yasiyofaa. Tunahitaji ushirikiano ulioimarishwa na Mamlaka za Kitaifa za Data zilizo na mizizi katika kuaminiana na kuwajibika. Maamuzi ya kuunda mifumo ya kukusanya data iliyoimarishwa na inayojumuisha zaidi na sera za kijamii zinahitaji jamii kuwa katikati, kujulisha jitihada za kujenga upya na kupona."

---

**Mati Soren,**
Bingwa wa Vijana wa kike aliye na umri wa miaka 26 katika Youth-led Digital Engagement Project (Mradi wa Ushirikisho Unaoongozwa na Vijana). Mshiriki wa jamii asili ya Santal, Gonoker Daing (Godagri, Rajshahi), Kaskazini-Magharibi mwa Bangladesh.



"Ripoti hii inadhihirisha kwamba COVID-19 imekuwa na athari isiyo na usawa. Ripoti hii pia inaonyesha kwamba data iliyotokezwa na/au iliyohalalishwa na Ofisi za Takwimu za Kitaifa hupuuza athari nyingi mbaya za janga la COVID-19 kwa watu ambao wametengwa hapa Bangladesh. Ukosefu wa watu ambao wametengwa katika data rasmi mara nyingi hutenga vikundi na watu katika jamii yangu kutoka kwa itikio la kitaifa la COVID-19. Data isiyo rasmi inayokusanywa na jamii na mashirika ya asasi za kiraia, inaweza kuongeza uwezo wa kuonekana wa watu ambao wametengwa ambao wanapuuzwa na data rasmi na kuboresha uelewaji wa mikakati yao ya kukabiliana. Ninatumaini kwamba ripoti hii itachochea washikadau watekeleze maitikio na maponyo ya COVID-19 yanayojumuisha zaidi, yakiongozwa na mapendekezo yaliyo katika ripoti hii."

---

**Sulayman AbdulMumuni Ujah,** mwanamume mwenye umri wa miaka 44 na mtetezi wa haki za walemavu viziwi na Afisa wa Mradi wa Kitaifa katika African Disability Forum (Mkutano wa Afrika wa Ulemavu), kutoka Abuja, Nigeria.



"Ripoti hii inaangazia changamoto zilizotokezwa na kutokuwa na data rasmi katika janga inayozingatia watu walio na ulemavu na data rasmi isiyotambua na kushughulikia mapengo muhimu na vizuizi vinavyokabiliwa na watu walio na ulemavu. Kama matokeo, ripoti hii inasaidia washikadau wote kutambua uhitaji wa kushughulikia mapengo na vizuizi na kurudia tena umuhimu wa serikali kutumia data iliyotenganishwa ya ulemavu ili kuunda programu na sera zinazotegemea uthibitisho. Kwa tumaini, washikadau wote watatekeleza kwa ukamili mapendekezo ya ripoti ili kuhakikisha ujumuishaji kamili wa watu walio na ulemavu katika uingiliaji kati wote wa COVID-19."

**Vappu Taipale,** mwanaharakati wa kike wa haki za watu wenye umri mkubwa zaidi mwenye umri wa miaka 81, kutoka Helsinki, Ufini.



"Serikali zimejaribu kadiri ya uwezo wao kutafuta suluhisho la COVID-19 linalowalinda na kuwategemeza raia – na uchumi wao. COVID-19, hata hivyo, imetokeza changamoto kwa kila mmoja. Hapa katika nchi za Nordic, watu wenye umri mkubwa zaidi mara nyingi huishi peke yao, wakiwa wamefungiwa katika ghorofa ndogo, bila wageni. Mashirika ya UN yameanza kuongea kuhusu 'janga la kivuli', kuongezeka kwa jeuri inayotokea nyumbani. Kuna kivuli kingine chenye giza zaidi ambacho hakishughulikiwi: watu wenye umri mkubwa zaidi kunyimwa kukutana na watu. Hapa ndipo civil society organisations (mashirika ya asasi za kiraia) yana jukumu muhimu la kutimiza. Civil Society Organisations (Mashirika ya asasi za kiraia) yamenasa mambo yaliyoshuhudiwa na watu wenye umri mkubwa zaidi ili kusaidia kuongoza itikio na ponyo la janga."

# Mapendekezo Yetu

Maitikio ya serikali kuelekea COVID-19 lazima yasaidie na kuimarisha jitihada za jamii zinazoshuhudia kutengwa ili kuzuia mpanuko zaidi wa ukosefu wa usawa na utanguzi wa maendeleo katika Sustainable Development Goals (SDGs) (Malengo ya Maendeleo Endelevu).

**Ili kuzuia ukosefu wa usawa kuongezeka kina kupitia mifumo ya data inayojumuisha zaidi, The Civil Society Collaborative on Inclusive COVID-19 (Ushirikiano wa Asasi za Kiraia katika Data Inayojumuisha ya COVID-19) inatoa wito wa:**

## Kutumia data kutoka kwa jamii na CSO kuarifu mipango na kufuatilia itikio na ponyo la COVID-19.

**YA MUDA MFUPI**

Vikosi vya kazi vya kitaifa vya COVID-19 na mabaraza sawia ya uratibu ya serikali yatafute kwa ukamilifu na kutumia data ya jamii na CSO ili kuarifu maendeleo na ufuatiliaji wa mipango na sera za itikio na ponyo la kitaifa na chini ya taifa.

**YA MUDA MFUPI**

Jamii na CSO huongeza ugawanyaji na usambazaji wa data inayohusiana na COVID-19 kulingana na mazoea bora zaidi, ikiambatana na mazungumzo yaliyo wazi ya mbinu zilizotumika, upungufu na nguvu zake.

## Utenganishaji wa haraka wa data ya COVID-19 ili kutambua, kushughulikia na kuripoti ukosefu wa usawa na kutanguliza uendelezaji wa ujumuishaji wa mifumo rasmi ya data.

**YA MUDA MFUPI**

Wizara za serikali na Ofisi za Takwimu za Kitaifa (NSOs) ziimarishe ukusanyaji, matumizi na kuripoti data ya visa, vifo na athari za kijamii na kiuchumi za COVID-19, ikiitenganisha kulingana na umri, ulemavu jinsia, eneo hususa, mapato, hali ya uhamiaji/kuhamishwa, utaifa au sifa nyinginezo zinazofaana katika muktadha wa kienyeji na kitaifa.

**YA MUDA MREFU**

NSO, kwa uratibu na idara za serikali, ziimarishe mifumo rasmi ya data ili ijumuishe wote na kuwa tayari kwa ajili ya majanga yajayo, kutia ndani kuongeza mifumo ya uandikishaji ya raia, kuzidisha kina cha utenganishaji wa data na kuongeza utokezaji na matumizi ya data ya ubora.

## Ushirikiano ulioimarishwa na mifumo ya uratibu baina ya serikali, jamii na CSO ili kuongeza matumizi ya data ya jamii na CSO.

**YA MUDA MFUPI**

NSO iteue kiongozi wa kiwango cha juu aliye na daraka la kufanya kazi na jamii na CSO ili kukusanya, kuchanganua na kutathmini ubora wa data ya jamii na CSO ili kufafanua zaidi changanuzi na ripoti zinazotolewa kwa kutumia data rasmi.

**YA MUDA MREFU**

NSO na idara nyinginezo za serikali zianzishe na kuimarisha ushirikiano wa data na vikundi vya kazi pamoja na jamii, CSO na watoaji wengine muhimu wa data husika isiyo rasmi (kama vile Taasisi za Haki za Kibinadamu) ili kuanzisha mifumo yenye matokeo na iliyo wazi ya kutokeza, kushiriki, kuchanganua na kutumia data ya jamii na CSO pamoja na data rasmi.

**YA MUDA MREFU**

NSO, jamii na CSO kufanya kazi pamoja ili kutokeza miongozo ya kitaifa na viwango vya ubora kwa ajili ya data ya jamii na CSO, na hivyo kutegemeza matumizi makamilifu ya data ya aina hiyo katika upangaji wa sera, utekelezaji na itikio la janga. Jamii na CSO zitathmini na kuripoti kuhusu ubora wa data yao.

---

## Kuharakisha uwekezaji katika utokezaji wa data ya jamii na CSO na uendelezaji wa mifumo rasmi ya data inayojumuisha zaidi.

**YA MUDA MFUPI NA MUDA MREFU**

Serikali za kitaifa na wafadhili wanapaswa kutia moyo, kuwezesha na kutenga fedha kwa ajili ya utokezaji wa data ya jamii na CSO ili kufanyiza programu zilizo na matokeo zaidi, zilizolengwa na kufikika zinazosaidia kushughulikia hali za jamii zinazoshuhudia kutengwa.

**YA MUDA MREFU**

Serikali na wafadhili kuongeza ufadhili kwa NSO na idara za serikali ili kuimarisha mifumo rasmi ya data yenye kina na inayojumuisha.

**YA MUDA MREFU**

Wafadhili kutegemeza ubadilishanaji wa ujuzi na kujenga uwezo baina ya NSO, jamii na CSO ili kuimarisha ubora wa data, usambazaji na matumizi.

**Kuendeleza ponyo la usawa la COVID-19 na kutimiza uwajibikaji kuelekea usiache yeyote nyuma, ushirikiano huu unatoa wito wa:**

## Watu ambao wameachwa nyuma wapewe kipaumbele katika itikio la COVID-19 na upangaji wa ponyo la muda mrefu, utekelezaji na upangaji wa bajeti.

**YA MUDA MFUPI**

Vikosi vya kazi vya kitaifa vya COVID-19 na mabaraza sawia ya uratibu ya serikali yatathmini kwa makini mikakati yote iliyopangwa na kupitishwa hivi karibuni ya itikio la COVID-19 ya chini ya taifa na ya kitaifa ili kuona ikiwa inaitikia kwa ukamilifu hali za watu ambao wametengwa.

**YA MUDA MREFU**

Serikali za kitaifa kuimarisha na kuboresha ulengaji wa hatua za ulinzi wa kijamii kwa kutegemea uchanganuzi unaokutanisha wa athari za kiuchumi za janga hili kwa watu ambao wametengwa.

**YA MUDA MREFU**

Serikali kuhakikisha mipango ya ponyo la kiuchumi na mikakati mingine ya kitaifa na chini ya taifa ya COVID-19, bajeti na mipango ya utekelezaji kutimiza kanuni ya kutoacha yeyote nyuma. Anzisha mizunguko zaidi ya utengenezaji wa bajeti inayoshirikisha katika viwango vya chini ya taifa na kitaifa ili kufuatilia na kupitia utekelezaji wa programu na ulengaji wa jamii zinazoshuhudia kutengwa.

---

## Mikakati ya kufanya maamuzi inayojumuisha na inayoshirikisha katika itikio na ponyo la COVID-19 na sera na programu za muda mrefu zaidi.

**YA MUDA MFUPI**

Vikosi vya kazi vya kitaifa vya COVID-19 na mabaraza sawia ya uratibu ya serikali yashirikiane na jamii na CSO katika kutokeza kwa pamoja mifumo ya uwajibikaji ili kutambua na kushirikisha wawakilishi wa watu ambao wametengwa ili kushiriki kikamilifu na kushiriki katika kufanya maamuzi na michakato ya utekelezaji.

**YA MUDA MREFU**

Wawakilishi wa jamii na CSO kuimarisha ushirikiano na miungano inayokutanisha katika viwango vya kienyeji, kitaifa na ulimwengu ili kutegemeza michakato ya kufanya uamuzi inayojumuisha na kunyoosha ushirikiano na serikali.

**YA MUDA MREFU**

Idara za serikali kutokeza kwa pamoja mifumo ya uratibu pamoja na jamii zinazoshuhudia kutengwa ili kuhakikisha uongozi na ushirikisho wao ulio kamili, wenye matokeo na usawa katika kufanya maamuzi ya kuunda, kutengeneza bajeti, utekelezaji na ufuatiliaji wa sera na programu.

# Soma ripoti kamili.

The Civil Society Collaborative on Inclusive COVID-19 (Ushirikiano wa Asasi za Kiraia katika Data Inayojumuisha ya COVID-19) husitawisha uwezekano wa data iliyotokezwa na jamii na Civil Society Organisations (CSOs) (Mashirika ya Asasi za Kiraia). Ushirikiano huu unalenga kuunda uelewaji wa jumla wa jinsi watu ambao wametengwa wameathiriwa na janga la COVID-19, itikio na ustahimilivu wao.

**bit.ly/UnequalPandemic**



© Sightsavers

#UnequalPandemic

**Wanachama wa Ushirikiano wetu:**

- actionaid
- Africa's Voices
- cbm global disability inclusion
- christian aid
- CIVICUS
- Consortium for Street Children
- development initiatives
- Global Partnership for Sustainable Development Data
- HelpAge International
- igh George and Tanya Ruff Institute of Global Homelessness
- iDMC internal displacement monitoring centre
- International Civil Society Centre
- International Rescue Committee
- Islamic Relief
- peace direct
- Plan International
- IMPACT Shaping practices Influencing policies Impacting lives
- Restless Development
- Save the Children
- Sightsavers
- Transparency International
- VSO
- World Vision